# MPANGO WA UTEKELEZAJI WA JUMUIA ZA WAAFRIKA VIKTORIA

## Muhtasari wa Lugha ya Kiingereza Kilicho Rahisi

**Kusoma mpango wote tembelea www.multicultural.vic.gov.au.**

**Mpango wa Utekelezaji wa Miaka 10 kwa Jumuia za Kiafrika una lengo la kujenga jumuiya za kuwapokea, kuboresha matokeo na kujenga fursa za kudumu kwa Wana Viktoria wenye asili ya Afrika.**

Mpango wa Utekelezaji umeandaliwa na jumuiya za ViKtoria za Kiafrika kwa Jumuia za Waafrika zinazoishi Viktoria

Uendelezaji wake uliongozwa na Kundi la Waafrika la Kikazi la Waziri (AMWG), kikundi cha watu 22 tofauti wenye asili ya Kiafrika, tangu Oktoba 2016 hadi Februari 2018. Wakati huu, mamia ya watu katika jumuiya za Afrika za Viktoria walitoa mawazo na maoni yao kusaidia kuandaa mpango huu.

Mpango wa Utekelezaji unashughulikia matatizo ambayo yana julikana. Mpango huu unalemnga kuimarisha na kuwasaidia watu kufanya maamuzi ambayo yanaboresha maisha yao.

## JUMUIA KUWA MSITARI WA MBELE KUONGOZA

Mpango wa Utekelezaji unawataka watu wa Jumuiya za Waafrika za Viktoria kuumiliki wenyewe, kuongoza na kuwa wahusika wa ufumbuzi. Inahitajika ushirikiano, rasilimali, utaalamu, uelewa na ujuzi wa kuleta mabadiliko ya kudumu.

Mpango wa Utekelezaji pia unazitaka Serikali pamoja na sekta za kiraia, kibinafsi, za kielimu, za kujitolea, kufikiri juu ya jinsi ambavyo wanaweza kushirikiana kwa karibu na jumuiya za Kiafrika ili kusaidia kuboresha ustawi.

Mpango wa Utekelezaji unasaidiwa na kanuni nne muhimu:

- Kuhusisha vipaji na ujuzi wa wana jumuia
- Kuwajibika
- Kufanya kazi kwa kushirikiana
- Kujenga kuleta mabadiliko ya kudumu

## KUSHUGHULIKA KULETA MABADILIKO YA KUDUMU

Mpango wa Utekelezaji unapendekeza hatua zaidi ya 250 katika maeneo sita yanayo lengwa.

Matendo yaliyopendekezwa yanalenga kujenga fursa kwa watu wote kujisikia kuishi, kushiriki kuchangia na kustawi.

Matendo pia yanaongezea kwenye kazi za kujenga, ambazo tayari zimeshafanywa na jumuiya, serikali na wengine kusaidia watu katika jumuia za Kiafrika za Viktoria.

## MALENGO SITA YA MPANGO WA UTEKELEZAJI

1. **Biashara**

   Kukuza uvumbuzi wa Waafrika wa Viktoria kwenye biashara na uwekezaji katika maeneo yote ya uchumi

2. **Ajira**

   Kuimarisha ujuzi na njia za kupata ajira za maana katika sekta zote za kazi

3. **Elimu na Mafunzo**

   Kujenga misingi imara ya kujifunza na ujuzi wa maisha

4. **Afya na Ustawi**

   Kuinua ustawi wa kijamii, kihisia na kimwili kwa watu wote

5. **Kuhusishwa na kuwezeshwa**

   Kuwaunga mkono watu kupata usawa, kupewa haki na na kuheshima

6. **Uongozi, ushirikiano na uhusiano**

   Kuchangia kwa Victoria Imara kupitia uongozi wa uhakika, jumuia za ushirikiano na uhusiano wa nguvu katika jamii pana.

# MUHTASARI WA MPANGO WA UTEKELEZAJI

## Mandhari tatu za kawaida

Kuna mandhari tatu ambazo ni za kawaida kwa maeneo yote ya kuzingatiwa. Hizi zitasaidia kuongoza utoaji wa malengo.

Ushiriki bora na huduma bora kwenye Mpango wa Utekelezaji

*Kuboresha upatikanaji, matumizi na ufanisi wa huduma kupitia ushiriki mkubwa wa wana jumuia*

Kujenga ustadi kupitia ushirikiano

*Kuunga mkono ushirikiano wenye nguvu na kutowa fursa za kujenga uwezo wa jumuia kuongoza na kuleta mafanikio*

Kuboresha ujuzi na ushahidi

*Kuimarisha ujuzi wa jumuiya na upatikanaji wa ushahidi unao onekana ili kuongoza matendo ya jumuia kwa siku zijazo*



# MAENEO YA KUZINGATIA NA MASOMO

Kila eneo linalo lengwa linaonyesha hatua ambazo zinaitikia maswala muhimu zaidi ambayo hupunguza ustawi wa kiuchumi na kijamii wa watu katika jumuiya za Kiafrika.

Zaidi ya nusu ya vitendo vyote zina lengo la kuwasaidia na kuwatia moyo vijana, na familia zao.

Kwa kuwa huu ni mpango wa miaka 10, baadhi ya matendo yatatolewa mapema, wakati mengine yatahitaji mipango zaidi na kutolewa baadaye.

## Namna ya Kuelekea mbele

Uwajibikaji wa mipango hii haisimamii tu upande wa serikali, au sehemu moja ya jamii.

Kuleta Mpango wa Utekelezaji utaweza kusimamiwa kupitia 'mbinu ya ushirikiano'. Hii ina maanaya kuwashirikisha watu na mashirika kutoka kwa jumuiya zote, ngazi zote za serikali na sekta zote katika kutoa matendo.

## Vipaumbele vya Utekelezaji

AMWG wamesema kuna mambo matatu muhimu ambayo yanafaa kuongoza njia inayoendelea.

1. Utawala Imara na ushirikiano
2. Kuhusisha kutoka kote Viktoria
3. Kupima, kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa kuhusu maendeleo

| MAENEO YANAYO LENGWA | MASOMOYALIYO CHAMBULIWA NA MATENDO YALIYOPENDEKEZWA | |
|---|---|---|
| BIASHARA | Biashara<br>Ujasiriamali na uvumbuzi | Mitandao ya biashara na ushirikiano<br>Biashara na uwekezaji |
| AJIRA | Utayarishaji kwa kazi<br>Wanao acha Shule mapema na wale walio maliza shule hivi karibuni<br>Upatikanaji wa kazi na kuajiriwa | Ustadi na ujuzi kutoka nchi za nje<br>Uhifadhi na uhamiaji wa kupanda juu |
| ELIMU NA MAFUNZO | Elimu ya watoto wachanga<br>Uhusiano kwenye elimu<br>Mipango kabla na baada ya shule<br>Watoto umri wa shule na vijana | Elimu ya watu wazima na kujifunza<br>Kazi za kupata ujuzi na kujitolea<br>Elimu ya juu na mafunzo ya ufundi |
| AFYA NA USTAWI | Magonjwa ya akili<br>Afya ya Mwili na magonjwa sugu<br>Vurugu za familia | Vijana walio katika hatari<br>Watu wakubwa na wazee<br>Kuimarisha familia |
| KUHUSIHWA NA KUWEZESHWA | Watu wageni wanao wasili<br>Watu wenye ulemavu<br>Watu wakubwa na wazee<br>Jinsia na uwezo wa Ujinsia | Watu katika Mfumo wa Sheria<br>Wanawake na usawa wa kijinsia<br>Ulinzi kwa watoto |
| UONGOZI, USHIRIKIANO NA UHUSIANO | Uongozi wa kwenye Jumuia<br>Kufundishana na muundo wa kusimamia<br>Ushirikiano katika jumuiya zote<br>Vijana | Miundombinu na vifaa<br>Vyombo vya habari<br>Kuzielewa sheria za Australia na Ushirikiano na mamlaka |

VICTORIA